**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UZINDUZI WA JENGO LA JIOLOJIA YA NGORONGORO-LENGAI (THE NGORONGORO LENGAI-GEOPARK)

**KARATU, ARUSHA**
**16 OKTOBA, 2025**

- ***Mhe. Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii, na Wahe. Mawaziri wote mliopo;***
- ***Mhe. Chen Mingjian, Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China Nchini Tanzania;***
- ***Mhe. Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Arusha;***
- ***Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, na Makatibu wakuu wote mliohudhuria;***
- ***Jen. (Mst.) Venance Mabeyo, Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi NCAA;***
- ***Ndg. Thomas Ole Sabaya, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha;***
- ***Mhe. Lameck Karanga Ng'ang'a, Mkuu wa Wilaya ya Karatu na Wakuu wote wa Wilaya mliopo;***
- ***Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Karatu;***
- ***Menejimenti, Maafisa na Askari wa NCAA;***
- ***Wageni Waalikwa;***
- ***Waandishi wa Habari;***
- ***Wahe. Wananchi;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**
Sina budi kuanza hotuba yangu, kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetujalia afya na kutuwezesha kukutana katika hafla hii ya uzinduzi rasmi wa jengo la Makumbusho ya Eneo la Hifadhi ya Urithi wa Kijiolojia la Ngorongoro – Lengai (The Ngorongoro-Lengai Geopark) linalotambuliwa na UNESCO. Aidha, namshukuru Mhe. Balozi, Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kumwalika Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgeni rasmi katika tukio hili muhimu. Kama mnavyofahamu, Mhe. Rais anaendelea na kampeni za uchaguzi Mkuu, hivyo amenipa heshima ya kumwakilisha. Pia, napenda kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. Amos Makalla na wananchi wa Mkoa wa Arusha, hususan Wilaya ya Karatu kwa mapokezi mazuri mliyonipa na ushiriki wenu katika hafla hii.

Vilevile, napenda kutumia hafla hii kuishukuru kwa dhati Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza miundombinu mbalimbali nchini, ikiwemo ujenzi wa Kituo hiki cha *Geopark* ya Ngorongoro - Lengai. Kupitia mradi huu, China imeendelea kuwa rafiki wa kweli katika safari yetu ya kukuza uhifadhi na utalii kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Tanzania na China zinajivunia uhusiano wa kirafiki na kidugu ulioanzishwa na waasisi wa mataifa haya mawili tangu mwaka 1964, ambapo hadi sasa yameendelea kushirikiana katika sekta za biashara, utamaduni, utalii, afya na uendelezaji wa miundombinu. **Asanteni sana Ndugu zetu wa China!**

***Wahe. Viongozi na Wananchi wenzangu;***

Kama mnavyofahamu, mwaka 2018 eneo hili la Hifadhi ya Ngorongoro lilitambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuwa eneo la Hifadhi ya Jiolojia ya Ngorongoro-Lengai, ambayo ni *Geopark* pekee katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na ya pili katika bara la Afrika. Kwa kutambua umuhimu wa uhifadhi wa historia na umuhimu wa Jiolojia ya Ngorongoro - Lengai, Serikali imedhamiria kuboresha na kulinda miundombinu yake. Hivyo, kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, tumeweza kujenga makumbusho haya ya kisasa, pamoja na kuboresha uhifadhi na huduma za utalii katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na maeneo mengine ya hifadhi ya jiolojia ya Ngorongoro-Lengai. Ni matumaini ya Serikali kuwa kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kukuza sekta ya utalii na kuvutia idadi kubwa ya watalii wa utamaduni. Hali kadhalika, mradi huu utawezesha upatikanaji wa taarifa za kijiolojia na hivyo kuifanya nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zilizopiga hatua katika aina hii ya utalii. *Geopark* hii ina manufaa makubwa kwani licha ya kutunza zana za kale, simulizi, maarifa asilia na tamaduni, itawezesha pia elimu ya jiolojia na mazingira kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kuwezesha tafiti za kiikolojia na mabadiliko yake. Aidha, kupitia *Geopark* hii, tutaweza kuimarisha ushirikiano na ubadilishanaji maarifa na taarifa kuhusu uhifadhi endelevu wa maliasili. Hivyo, Serikali inawakaribisha watafiti na wabobezi wa masuala ya jiolojia kutembelea kituo hiki kwa lengo la kujifunza na kufanya tafiti zaidi za kijiolojia katika maeneo haya.

***Wahe. Viongozi na Wananchi wenzangu;***

Sekta ya utalii ni mojawapo ya sekta zenye mchango mkubwa sana kwa Taifa, ikiwa ni chanzo kikubwa cha fedha za kigeni. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, mchango wa sekta hii ni takriban 17% ya pato la Taifa. Aidha, kufuatia janga UVIKO 19 kati ya mwaka 2019 hadi 2020, sekta hii iliathiriwa, ambapo idadi ya watalii nchini ilishuka kwa takriban 59%, kutoka watalii 1,527,230 mwaka 2019 hadi watalii 620,867 mwaka 2020. Hata hivyo, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za makusudi ili kuhakikisha inaboresha huduma za utalii, ikiwemo kutengeneza filamu mbili maarufu za ***"Tanzania: The Royal Tour***" (2022) na ***"Amazing Tanzania"*** (2024). Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuboresha miundombinu mbalimbali ya utalii hususan barabara, hoteli, nyumba za kulala wageni, viwanja vya ndege na nyinginezo. Pia, kurahisisha upatikanaji wa visa, kuimarisha usalama wa watalii, kuwekeza katika maendeleo ya rasilimaliwatu na kuimarisha taswira ya nchi yetu duniani*.* Ujenzi wa Kituo hiki cha *Geopark* ya Ngorongoro-Lengai pia ni sehemu ya jitihada hizo. Matokeo ya jitihada hizi ni pamoja na kuvutia watalii wengi zaidi, ambapo mwaka 2024 tulipokea jumla ya watalii 5,360,247. Aidha, mapato yatokanayo na shughuli za utalii yaliongezeka kutoka Shilingi millioni 700 mwaka 2020, hadi Shilingi bilioni 4.0 mwaka 2024. Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2025 – 2030) imeweka lengo la kuongeza idadi ya watalii kutoka millioni 5.3 hivi sasa, hadi kufikia

watalii millioni 8 kwa mwaka, ifikapo mwaka 2030. Hivyo, wito wangu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wote wa utalii ni kuendeleza jitihada za kuvutia watalii kwa njia mbalimbali husussan kwa kutangaza vivutio vyetu.

***Wahe. Viongozi na Wananchi wenzangu;***

Kabla ya kumalizia hotuba yangu, napenda kuweka msisitizo katika masuala machache ambayo naamini ni muhimu katika kukuza utalii nchini, hususan utalii wa historia:

***Kwanza,*** ni kuhusu utunzaji wa mazingira na uendelevu wa shughuli za utalii. Kiwango cha uharibifu wa mazingira nchini ni kikubwa, kiasi cha kuvuruga ikolojia na kutishia ustawi wa shughuli za utalii. Kutokana na uharibifu huo tunashuhudia muingiliano kati ya wanyamapori na binadamu unaopelekea athari kubwa zaidi, vikiwemo vifo na uharibifu wa makazi na mazao. Hivyo, suala la utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi linapaswa kupewa kipaumbele katika uendelezaji na ukuzaji utalii.

***Pili,*** ni kuhusu utunzaji wa miundombinu ya utalii. Ujenzi wa miundombinu bora na ya kisasa ni sehemu ya utekelezaji wa mipango sera za Serikali za kukuza utalii nchini. Ninaihimiza Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuhakikisha kuwa miundombinu hii inatunzwa na kutumika kama ilivyokusudiwa. Vilevile, ni muhimu kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha ukarabati na matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu na mifumo iliyowekwa katika jengo hili. Tukumbuke Wahenga walisema "kitunze kidumu".

***Tatu,*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake ikiwemo Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, ihakikishe inatoa mafunzo stahiki kwa watumishi watakaohudumu katika eneo hili ili kuwawezesha watumishi hao kutumia mifumo iliyopo na kutoa huduma kwa ufasaha na ufanisi. Kwa kadri itakavyowezekana, mafunzo hayo yashirikishe wadau wa utalii ambao wana mchango katika kutuletea wageni watakaokuja kujifunza kupitia utalii wa mambo mbalimbali yaliyopo katika kituo hiki.

***Nne,*** mojawapo ya majukumu ya *Geopark* ni kuinua hali za jamii zinazoizunguka (empowering communities). Ninaitaka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kufanya jitihada za makusudi kushirikisha jamii inayozunguka eneo hili katika shughuli za uhifadhi wa eneo hili, zikiwemo mila na tamaduni zake.

***Tano,*** ni wito kwa Watanzania, hususan katika Wilaya za mkoa wa Arusha na mikoa mingine nchini, kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vyetu na maeneo ya kihistoria ili kujifunza na kujionea utajiri mkubwa tuliojaliwa. Kituo hiki kilichozinduliwa leo ni hazina kubwa ya maarifa na mojawapo ya utajiri wetu.

***Wahe. Viongozi na Wananchi wenzangu;***

Ninapenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kupongeza jitihada za uhifadhi na ukuzaji wa shughuli za utalii zinazofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na wadau wengine. Pia, kwa usimamizi wa karibu wa miradi mbalimbali ukiwemo huu uliozinduliwa leo na kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa viwango vya juu. Aidha, naipongeza kampuni ya *China 25 Bureau Group Company Ltd* kwa kujenga mradi huu kwa ubora unaoakisi thamani ya fedha.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninayo heshima kutamka kuwa jengo la *Geopark* ya Ngorongoro-Lengai limezinduliwa rasmi.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**